# KUUWEZA

# WAKATI UJAO

**“Akili za kujua nini cha kufanya kwa majira ya sasa na yanayokuja.”**

**Pastor, Tony Osborn**

**© April 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

# YALIYOMO:

SHUKRANI........................................................................ vi

UTANGULIZI ..................................................................... viii

Lengo kuu la kuandika kitabu hiki. ........................................... ix

*Sura ya 1:* ........................................................................ 1

WAKATI UJAO ................................................................... 1

1.1 Nyakati na Majira............................................................ 1

1.2 Wakati ujao ni nini? ......................................................... 6

1.3 Namna ambazo Mungu hutumia kutuonyesha mambo ya wakati ujao. ........................................................................ 18

1.4 Siri za Kiroho za wakati ujao. ........................................... 32

1.5 Tunauwezaje wakati ujao?................................................ 42

1.6 Umuhimu wa kujua na kuyaweza mambo ya wakati ujao. ......... 46

*Sura ya 2:* ........................................................................ 53

KANUNI ZA KUUWEZA WAKATI UJAO ................................. 53

2.1 Kujazwa Hekima, Maarifa na Ufahamu wa kiungu kwa ajili ya kuiweza kesho............................................................. 53

2.2 Kuwa mtu bora kila siku na katika kila eneo la maisha yako. .... 75

2.3 Kujazwa na akili ya Kimungu (Divine Intelligence). ................. 77

2.4 Kumjenga na kumtengeneza mtu wa ndani. ............................ 83

*Sura ya 3:* ........................................................................ 85

SILAHA ZA KUUWEZA WAKATI UJAO .................................... 85

3.1 Kuokoka ........................................................................ 86

3.2 Ubatizo wa Maji mengi. ................................................ 98

3.3 Kujazwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu. .......................... 101

3.4 Kunena kwa lugha. ........................................................ 117

3.5 Kusoma na kutafakari Neno la Mungu. ................................. 119

3.6 Kufunga na kuomba. ...................................................... 127

3.7 Imani. ......................................................................... 138

3.8 Ufunuo......................................................................... 155

3.9 Sadaka ........................................................................ 158

3.10 Ushirika wa Meza ya Bwana. ........................................... 184

3.11 Roho ya Utulivu. .......................................................... 190

3.12 Kibali na Neema ........................................................... 192

*Sura ya 4:* ........................................................................ 198

KUJIANDAA KWA AJILI YA WAKATI UJAO .......................... 198

4.1 Maandalizi ya Kiroho. .................................................... 198

4.2 Maandalizi ya Kimwili. .................................................. 204

4.3 Maandalizi ya Kiakili. .................................................... 207

*Sura ya 5:* ........................................................................ 213

KUUWEZA WAKATI UJAO ENEO LA BIASHARA NA KAZI213

*Sura ya 6:* ........................................................................ 224

KUUWEZA WAKATI UJAO ENEO LA UCHUMI NA FEDHA ........................................................................................... 224

*Sura ya 7:* ........................................................................................ 232

KUUWEZA WAKATI UJAO ENEO LA MAHUSIANO, NDOA NA MALEZI ........................................................................ 232

*Sura ya 8:* ........................................................................................ 241

KUUWEZA WAKATI JAO KAMA TAIFA AU NCHI ................ 241

*Sura ya 9:* ........................................................................................ 247

MAOMBI YA KUTANGAZA NA KUKIRI KESHO ILIYO BORA ........................................................................................... 247

HITIMISHO: ............................................................................. 252

# SHUKRANI:

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo na hekima kubwa ameniwezesha kukiandika kitabu hiki kuanzia mwanzo mpaka mwisho na kwa kadri ya wingi wa hekima na maarifa yake kitabu hiki kikakamilika.

Siri zilizoandikwa humu kwa uwezo wa Roho wa Mungu zitakusaidia na kukuongoza na kukuonyesha nini unapaswa kufanya ili kuuweza wakati ujao ambao hakuna ajuaye mambo gani yanapaswa kutokea hapo baadae isipokuwa kwa wale tu waliofunuliwa na Roho wa Mungu.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Mhubiri 3:10-11**

**"Nimeiona taabu ambayo Mungu amewapa wanadamu, ili kutaabika ndani yake.**

**Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake; tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao; ila kwa jinsi mwanadamu asivyoweza kuivumbua kazi ya Mungu anayoifanya, tangu mwanzo hata mwisho."**

Neno hili linatuonyesha ya kuwa Mungu aliweka majira na nyakati ili kuongoza maisha yetu na kuwa kila jambo zuri ndani ya maisha ya mwanadamu ameweka kila moja kwa wakati wake.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa mafunuo na maombi yote yahusuyo somo la majira na nyakati na ni kwa njia zipi tutajiandaa kuuweza na kuutawala wakati unaokuja.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini, kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu.

Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini kile kitu na huduma Mungu ameweka ndani yangu.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

*Amen……………………*

***~Pastor Tony Osborn***

# UTANGULIZI:

Moja ya mbinu kubwa ambayo iliyasaidia majeshi mengi duniani kushinda vita zao ni kuwatuma baadhi ya watu kwa siri ili kwenda kupeleleza katika nchi ya adui na kujua wao wamejipanga vipi kupigana vita yao ili wao watafute na waende na mbinu bora zaidi ili wawashinde katika uwanja wa vita.

Kwa maana nyingine walitamani kujua adui zao walipanga nini na wamejiandaa vipi kupigana vita yao wakati wa vita unapokuja.

**Yoshua 2:1**

**“Yoshua, mwana wa Nuni, akawatuma watu wawili kutoka Shitimu kwa siri, ili kupeleleza, akawaambia, enendeni mkaitazame nchi hii, na Yeriko. Wakaenda wakafika nyumbani kwa kahaba mmoja jina lake aliitwa Rahabu, wakalala huko.”**

Wakati nilivyokuwa naendelea kutafakari Mungu akanifunulia siri kubwa sana juu ya majira na nyakati. Akanifundisha kuwa; maisha yetu hapa duniani sisi tuliokoka ni kama wanajeshi ambao tupo vitani na vita hii itaisha siku ambayo Yesu atarudi na kuwachukua watu wake. Akanifundisha tena ya kuwa; ili watu wa Mungu waweze kushinda katika kila eneo la maisha yao ni lazima wajifunze namna ya kuuweza na kuumiliki wakati ujao.

Mungu akanionyesha namna ambavyo watu wa ufalme wa giza wanakesha usiku na mchana ili kukamilisha ajenda zao na mipango yao ya wakati ujao.

Kuna mambo mabaya leo hii yanatokea katika uso wa nchi lakini ni mambo ambayo yalipangwa na kuandaliwa miaka ya nyuma kabla hata ya wakati huo haujafika na kabla hata ya hayo mambo hayajatokea.

Hii ikanionyesha ya kuwa; inawezekana kabisa sisi leo hii tukajiandaa na kujipanga kuitawala na kuimiliki kesho zetu kabla shetani hajaiba au kuharibu kesho zetu.

## Lengo kuu la kuandika kitabu hiki.

Kitabu hiki nimekiandika nikiwa na malengo makuu mawili;

i. **Kuwaandaa watu wa Mungu kiroho, kimwili na kiakili kuukabili wakati ujao.**

Ili kuwa na ushindi na mafanikio kwa wakati unaokuja unahitaji wewe binafsi kuwa na maandalizi ya kutosha ili kukuwezesha na kukusaidia kushinda.

Usipokuwa na maandalizi ya kutosha maana yake wewe utashindwa vita. Watu wote ambao wanashindwa vita zao kwa namna moja au nyingine walikosa kuwa na maandalizi mazuri juu ya kesho zao.

Maandalizi yako ya kutosha ndio ambayo yatakupa ujasiri wa kuwa na kesho iliyo bora.'

Ni kweli tunahitaji kuwa na imani kubwa katika kuuweza wakati ujao lakini Neno la Mungu linasema kuwa imani bila matendo imekufa kwa maana yake ili imani yako ya ushindi juu ya wakati unaokuja ifanye kazi lazima ufanye matendo ambayo yatakuandaa na yatakusogeza karibu na ushindi wako.

Tunajiandaa sio kwa sababu tunajua kesho yetu itakuwaje ila tunajiandaa kwa sababu hatujui nini tunahitajika kuwa nacho nyakati zijazo.

Unamkumbuka Daudi?

Daudi alivyokuwa anachunga kondoo za baba yake, alikuwa akipigana na simba na dubu waliokuwa wanajaribu kula kondoo bila ya yeye kujua kuwa hayo yalikuwa ni maandalizi kwa ajili ya kupigana na Goliati.

Vipi kama angeamua tu kukimbia akaacha kondoo waliwe?

Kwahiyo, hiki kitabu nimekiandika kwa ajili ya kumuandaa mtoto wa Mungu kuikabili kesho bila ya kuwa na hofu au mashaka ya mambo yanayoendelea duniani bali kuwafanya kesho zao kuwa kesho zenye ushindi na mafanikio makubwa.

**ii. Kuwaonyesha watu wa Mungu njia na mbinu ambazo zitawasaidia kuweza na kushinda wakati ujao.**

Nimeandika kitabu hiki pia ili kuwasaidia watoto wa Mungu kwa kuwapa mbinu, njia na siri ambazo kama wakizitumia wataweza kuushinda wakati ujao.

Wewe kama mtoto wa Mungu upo katika vita kali sana katika ulimwengu wa Roho na kazi kubwa ya adui ni kuhakikisha kuwa anakupoteza au anakupeleka katika njia za upotevuni ili wewe usiweze kufikia kesho yako iliyo bora.

Kwahiyo wakati shetani anapambana kuandaa mipango kwa ajili ya kuharibu ndoa yako, biashara yako, huduma yako na maisha yako ya baadae wewe pia unatakiwa kupambana kuhakikisha unavaa silaha za vita za Kimungu na kutumia siri na njia zilizomo katika kitabu hiki ili uweze kushinda.

### iii. Kuwapa watoto wa Mungu akili za kujua mambo yanayowapasa kuyafanya kwa wakati huu na ule unaokuja.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**1Nyakati 12:32**

**“Na wa wana wa Isakari, watu wenye akili za kujua nyakati, kuyajua yawapasayo Israeli wayatende; vichwa vyao walikuwa watu mia mbili na ndugu zao wote walikuwa chini ya amri yao.”**

Ili kuuweza wakati ujao ni lazima watoto wa Mungu wawezeshwe kwa kupewa akili ya kiungu ambayo itawawezesha kujua ni mambo gani wanayotakiwa kuyafanya kwa majira waliopo au kwa majira yanayokuja.

usipojua nini inakupasa kufanya ni rahisi sana wewe kushindwa na mazingira na hali zozote za wakati unaokuja, hivyo hiki kitabu kitakuwezesha wewe na kuitia akili yako nuru ili ujue yote yanayokupasa kutenda kwa majira na nyakati husika.

Ninaamini baada ya kumaliza kusoma kitabu hiki utakuwa umejazwa na hekima na ufahamu wa kutosha wa ni kwa namna gani utaweza kuuweza na kushinda wakati unaokuja.

Mungu akubariki sana na karibu kusoma kitabu hiki….

***~Pastor Tony Osborn.***

## *Sura ya 1:*

## WAKATI UJAO

### 1.1 Nyakati na Majira.

Kwa maana zilizopo katika kamusi za kingereza na kiswahili maneno haya mawili yamebeba maana tofauti kidogo japo yanaonekana kama yanataka kufanana.

Nyakati~ Hii humaanisha muda wa kawaida wa kila siku mfano; asubuhi, mchana, jioni na usiku.

Majira~ Hii humaanisha vipindi au misimu ndani ya nyakati yaani ndani ya nyakati (muda) ndipo yanapopatikana majira na kila majira yana chanzo na ukomo wake.

Katika ulimwengu wa Roho haya maneno yamebeba maana ileile tunayojifunza huku duniani.

Moja ya kitu cha thamani sana ambacho Mungu alimpa kila mwanadamu ni muda na mafanikio au kufeli kwa mtu yeyote yule kumefichwa ndani ya muda. Maana yake kuna siri kubwa sana kiroho iliyojificha nyuma ya nyakati na majira na kama ukiweza kuijua siri hii basi ni rahisi sana wewe kuiweza kesho yako.

Maisha ya mwanadamu yeyote yule yamefungwa katika majira na nyakati.

Tunasoma katika kitabu cha;

**Mhubiri 3:1-9**

Kuuweza wakati ujao. **“Kwa kila jambo kuna majira yake, na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu.**

**Wakati wa kuzaliwa, na wakati wa kufa; wakati wa kupanda, na wakati wa kung’oa yaliyopandwa;**

**Wakati wa kuua, na wakati wa kupoza; wakati wa kubomoa, na wakati wa kujenga;**

**Wakati wa kulia, na wakati wa kucheka; wakati wa kuomboleza, na wakati wa kucheza;**

**Wakati wa kutupa mawe, na wakati wa kukusanya mawe; wakati wa kukumbatia, na wakati wa kutokumbatia;**

**Wakati wa kutafuta, na wakati wa kupoteza; wakati wa kuweka, na wakati wa kutupa;**

**Wakati wa kurarua, na wakati wa kushona; wakati wa kunyamaza, na wakati wa kunena;**

**Wakati wa kupenda, na wakati wa kuchukia; wakati wa vita, na wakati wa amani.**

**Je! Mtendaji anayo faida gani katika yale anayojishughulisha nayo?”**

Kwahiyo kila mmoja wetu maisha yake yote yamefungwa katika majira na nyakati. Ijapokuwa wote tumepewa muda unaofanana lakini kila mmoja ana majira yake ya kujiliwa.